# Kusoma
## Kitabu cha Mwanafunzi

**Darasa la Kwanza**
**Kitabu cha Pili**




Taasisi ya Elimu Tanzania

# Kusoma

## Kitabu cha Mwanafunzi

## Darasa la Kwanza

## Kitabu cha Pili



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI
NA TEKNOLOJIA

*Cheti cha Ithibati*

Na. 4

Jina la Chapisho: Kusoma Kitabu cha Mwanafunzi Darasa la Kwanza Kitabu cha Pili

Mchapishaji: Taasisi ya Elimu Tanzania

Mwandishi: Taasisi ya Elimu Tanzania

ISBN: 978 - 9976 - 61 - 704 - 7

Kitabu hiki kimeidhinishwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia tarehe 19 Mwezi Januari Mwaka 20 18 kuwa kitabu cha Kiada kwa ajili ya Darasa la Kwanza katika ngazi ya elimu ya Msingi nchini Tanzania kulingana na Muhtasari wa mwaka 2015.

**Dkt. Edicome Cornel Shirima**
Kaimu Kamishna wa Elimu.

## Taasisi ya Elimu Tanzania

© Taasisi ya Elimu Tanzania, 2018

Toleo la kwanza 2018

ISBN 978 - 9976 - 61 - 704 - 7

Taasisi ya Elimu Tanzania
S.L.P. 35094
Dar es Salaam

| | |
|---|---|
| Simu | +255 22 2773005 / +255 22 2771358 |
| Faksi | +255 22 2774420 |
| Baruapepe | director.general@tie.go.tz |
| Tovuti | www.tie.go.tz |


Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kurudufu, kuchapisha, kutafsiri wala kukitoa kitabu hiki kwa namna yoyote ile bila idhini ya maandishi ya Taasisi ya Elimu Tanzania.

# Yaliyomo

Utangulizi....................................................iv

Shukurani.....................................................v

1. Ninapenda Shule ......................................1

2. Paka.........................................................2

3. Maji..........................................................3

4. Bakari.......................................................4

5. Kuku na Mwewe.........................................5

6. Mtoto Mtoro..............................................7

7. Maua.........................................................9

8. Matunda..................................................10

9. Baba ni Mvuvi..........................................11

10. Mwalimu Furaha.....................................12

11. Mwili Wangu .........................................13

12. Chakula cha Jioni....................................14

# Utangulizi

Kujua kusoma ni muhimu katika kujifunza. Ukijua kusoma utaweza kujifunza mambo mengi. Utaweza pia kumudu masomo yako mengine unayofundishwa shuleni.

Kitabu hiki kitakuwezesha kujua kusoma vizuri. Ukisoma kitabu hiki utaweza kusimulia matukio na hadithi. Vilevile utaweza kusoma kwa ufasaha na ufahamu.

Kitabu hiki kina maswali na mazoezi mbalimbali. Jibu maswali na kufanya mazoezi yaliyomo kitabuni. Iwapo utashindwa kujibu maswali au mazoezi waulize wenzako. Unaweza pia kuwauliza wazazi, walezi au walimu wako.

# Shukurani

Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) inatambua na kuthamini mchango muhimu wa washiriki waliofanikisha uandishi na maandalizi ya kitabu hiki.

TET inatoa shukurani za dhati kwa mchango uliotolewa na wataalamu wote walioshiriki kutayarisha kitabu hiki wakiwemo wachapaji, wasanifu, wahariri, wachoraji na wapiga chapa. Pia, inatoa shukurani kwa shule zote zilizoshiriki katika ujaribishaji wa maudhui na uhariri wa kitabu hiki.

Aidha, Taasisi inatoa shukurani za pekee kwa Shirika la “Global Partnership for Education (GPE)” kupitia Mradi wa Kukuza Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) uitwao “Literacy and Numeracy Education Support (LANES)” kwa ufadhili wao uliofanikisha kazi ya kutayarisha na kuchapa kitabu hiki.

Mwisho, Taasisi inatoa shukurani za pekee kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kusimamia kwa ukaribu zoezi zima la uandishi wa kitabu hiki.

**Dkt. Aneth A. Komba**
**Mkurugenzi Mkuu**
**Taasisi ya Elimu Tanzania**

# 1. Ninapenda Shule

Jina langu ni Mariamu. Ninapenda shule. Siku ninayokwenda shuleni ninaamka mapema sana. Ninapiga mswaki na kuoga. Kisha ninakausha mwili kwa taulo na kupaka mafuta. Halafu ninavaa sare yangu ya shule. Mama ananipa uji. Kisha baba ananipeleka shuleni. Shuleni ninakutana na watoto wengi. Kengele inapogongwa wote tunasimama mstarini. Baada ya kusimama mstarini tunaingia darasani. Mwalimu anasisitiza kuwahi shuleni kila siku.




## Zoezi

**Jibu maswali haya.**

1. Mariamu hufanya nini kabla ya kwenda shuleni?
2. Kwa nini Mariamu hupiga mswaki?
3. Nani humpeleka Mariamu shuleni?

## 2. Paka

Paka ni mnyama mzuri na mpole. Anafugwa na binadamu. Paka akitunzwa vizuri anakuwa na tabia nzuri. Sisi tunafuga paka nyumbani kwetu. Jina la paka wetu ni Pusi. Asubuhi Pusi hunywa maziwa. Mchana anakula chakula laini. Pusi ana sahani yake ya chakula. Pusi ana sanduku la kupumzikia mchana. Usiku huzunguka huku na huko kutafuta panya. Pusi akilia nyau! Nyau! Panya wote hukimbia na kujificha. Juzi usiku Pusi alikamata panya.




### Zoezi

**Jibu maswali haya.**

1. Kwa nini watu hupenda kufuga paka?
2. Paka wetu anaitwa nani?
3. Mchana Pusi anakula nini?
4. Pusi akilia nyau! Nyau! Panya hufanya nini?

# 3. Maji

Maji ni kitu muhimu sana. Watu, wanyama, ndege na mimea huhitaji maji. Kijijini kwetu mvua haijanyesha kwa muda mrefu. Mito na visima vya asili vimekauka. Baba amechimba kisima kirefu. Tunapata maji karibu na nyumbani. Hatuna tena shida ya maji. Watu wengine pia wanapata maji katika kisima chetu.



## Zoezi

**Jibu maswali haya.**

1. Viumbe gani vinahitaji maji?
2. Tunapata maji kutoka wapi?
3. Taja faida za maji?

# 4. Bakari

Bakari ana miaka sita. Anaishi kijijini na wazazi wake. Bakari ana tabia nzuri. Yeye ni mtii na msikivu. Ana heshima kwa watu wote. Anapenda kufanya kazi kwa bidii na kuwasaidia wengine. Bakari ana upendo kwa rafiki zake. Watoto wadogo wanampenda Bakari kwa ukarimu wake. Hapendi ugomvi. Mara nyingi huwaamua wenzake wanapogombana. Kila mtu anayemfahamu Bakari anampenda.




## Zoezi

**Jibu maswali haya.**

1. Bakari ana miaka mingapi?
2. Bakari anaishi na nani?
3. Taja tabia ya Bakari.
4. Kwa nini watoto wadogo wanampenda Bakari?

## 5. Kuku na Mwewe

Kuku na Mwewe walikuwa majirani. Siku moja kuku alikwenda kwa mwewe kuazima sindano. Alitaka kushona nguo za watoto wake. Mwewe akampa lakini akamwambia, asiipoteze. Kuku akakubali. Baada ya kushona nguo sindano ilipotea. Jioni mwewe alifika nyumbani kwa kuku kuchukua sindano yake. Kuku akaanza kuitafuta. Alichakura kwa kucha zake lakini sindano haikuonekana. Mwewe alikuwa juu ya mti akimtazama kwa hasira. Mwisho akamvamia ili ampige. Kuku akakimbia. Badala yake mwewe akachukua kifaranga cha kuku. Tangu hapo kuku na mwewe wakawa maadui.



## Zoezi la 1

**Jibu maswali haya.**

1. Jirani wa kuku alikuwa nani ?
2. Kuku alimkosea nini mwewe?
3. Kuku alichakura kutafuta nini?
4. Kwa nini mwewe na kuku ni maadui?

## Zoezi la 2

Simulia hadithi yoyote unayoifahamu.

# 6. Mtoto Mtoro

Baraka alikuwa anasoma darasa la kwanza. Alianza tabia mbaya ya kutoroka shuleni. Alikuwa akienda porini kuwinda ndege. Alitumia manati kuwindia ndege. Kila siku wenzake wanaporudi nyumbani yeye pia hurudi. Wazazi wake hawakujua kuwa mtoto wao haendi shuleni. Wenzake walijifunza kusoma, kuandika na kuhesabu. Baraka hakujifunza chochote. Siku moja baba yake alimpa kitabu asome.

Baraka hakuweza kusoma neno hata moja. Siku hiyo baba yake alipata barua kutoka shuleni. Alipoisoma aligundua kuwa mtoto wake ni mtoro. Akampa onyo. Tangu siku hiyo Baraka akawa anakwenda shuleni. Sasa anajua kusoma, kuandika na kuhesabu.



## Zoezi

**Jibu maswali haya.**

1. Baraka alikuwa na tabia gani?
2. Baraka alitumia nini kuwindia ndege?
3. Baba yake Baraka alipata barua kutoka wapi?
4. Hasara za kutoroka shuleni ni zipi?

# 7. Maua

Mama amepanda maua mengi. Amepanda maua ya rangi mbalimbali kuzunguka nyumba yetu. Kuna maua meupe, mekundu na ya njano. Maua yanaifanya nyumba yetu ipendeze. Mama anayapalilia na sisi tunamsaidia. Pia tunamwagilia maua kila siku. Kuna wadudu wanaopenda maua. Wadudu hao ni nyuki na vipepeo. Nyuki na vipepeo hutafuta chakula kwenye maua.



## Zoezi

**Jibu maswali haya.**

1. Mama amepanda nini kuzunguka nyumba?
2. Watoto humsaidia mama kufanya nini?
3. Nani anapalilia bustani ya maua nyumbani?
4. Taja rangi za maua ya bustani ya mama.

## 8. Matunda

Nyumbani kwetu kuna bustani ya miti ya matunda. Miti hiyo imezaa matunda mengi sana. Matunda hayo ni mapera, machungwa, maembe na mapapai. Tunatunza bustani yetu kwa zamu. Watoto wengi hupenda matunda. Wakati mwingine tunachuma na kula matunda. Matunda yanatusaidia kulinda mwili na kuongeza damu.



### Zoezi

**Jibu maswali haya.**

1. Nyumbani kwetu kumepandwa miti ya nini?
2. Taja matunda yaliyopo katika bustani yetu.
3. Taja aina nyingine za matunda unayoyafahamu.
4. Eleza faida za kula matunda.

## 9. Baba ni Mvuvi

Mimi ninaitwa Musa. Baba yangu ni mvuvi. Kila siku baba anakwenda mtoni kuvua samaki. Huchukua ndoana anapokwenda mtoni. Siku za mapumziko mimi humsaidia baba kuvua samaki. Jioni huwa tunarudi na samaki wengi. Samaki ni watamu sana. Samaki ni chakula bora. Mimi, baba na mama tunapenda sana kula samaki. Mdogo wangu Upendo anapenda kula nyama ya kuku.



### Zoezi

**Jibu maswali haya.**

1. Baba anakwenda mtoni kufanya nini?
2. Baba anatumia nini kuvua samaki?
3. Kwa nini tunakula samaki?
4. Upendo anapenda nini?

# 10. Mwalimu Furaha

Furaha ni mwalimu wa darasa la kwanza. Jana aliwafundisha kuhesabu, kusoma na kuandika. Leo mwalimu Furaha anawasimulia hadithi. Wanafunzi wanasikiliza hadithi kwa makini. Wanafurahia sana kusimuliwa hadithi. Kesho atawafundisha michezo.





## Zoezi

**Jibu maswali haya.**

1. Mwalimu wa darasa la kwanza anaitwa nani?
2. Mwalimu anawasimulia nini wanafunzi?
3. Wanafunzi wanapenda nini?
4. Mwalimu Furaha kesho atawafundisha nini wanafunzi?

# 11. Mwili Wangu

Mwili wangu umegawanyika katika sehemu mbalimbali. Nina kichwa, macho, pua na masikio. Vilevile nina mdomo, mikono, miguu na tumbo. Kila sehemu ina kazi yake. Macho huona vitu mbalimbali. Pua hunusa. Mdomo huzungumza na kula chakula. Mikono hushika vitu. Masikio husikia. Ninatembea na kukimbia kwa miguu. Tumbo hupokea chakula. Ninaupenda mwili wangu. Ninautunza vizuri.



## Zoezi


**Jibu maswali haya.**

1. Taja sehemu za mwili zilizooneshwa kwa mishale.
2. Kazi ya miguu ni nini?
3. Taja kazi ya tumbo.

## 12. Chakula cha Jioni

Mimi ninaitwa Tatu. Mdogo wangu anaitwa Sudi. Saa ya chakula tunakaa mezani na kula pamoja. Mara nyingi, jioni tunakula wali na maharage. Mimi ninapenda zaidi kula ugali, maharage na mchicha. Mdogo wangu anapenda sana wali na maharage. Kabla ya kula ninanawa mikono vizuri. Sudi naye hunawa mikono yake vizuri.

Wazazi wanasema tusizungumze wakati wa kula. Baada ya kula tunaondoa vyombo. Tunasafisha meza na kunawa mikono kisha tunasema asante. Tunawaaga wazazi wetu na kwenda kulala. Wazazi wanatufundisha tabia njema.




### Zoezi


**Jibu maswali haya.**


1. Mara nyingi Sudi na Tatu wanakula nini jioni?
2. Mdogo wake Tatu anapenda kula nini?
3. Kwa nini unanawa mikono kabla ya kula ?

**Vitabu vingine kutoka**
**Taasisi ya Elimu Tanzania**


## Darasa la Kwanza
















## Darasa la Pili















## Darasa la Tatu















ISBN 978-9976-61-704-7